JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA NA USIMAMIZI WAKE

***(Mada iliyoandaliwa kwa ajili ya Semina ya Madiwani, Januari 2006)***

**Januari, 2006**

# FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA NA USIMAMIZI WAKE

***(Mada iliyoandaliwa kwa ajili ya Semina ya Madiwani, Januari 2006)***

## Utangulizi

1. Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji ni serikali kamili katika maeneo yao. Sifa mojawapo ya serikali yoyote ni kwamba inakuwa na uwezo wa kupata na kutumia fedha. Serikali hupata fedha kwa kuwatoza raia wake kodi, ushuru na ada mbalimbali.

2. Hali kadhalika, Halmashauri za Miji na Wilaya zina madaraka ya kutoza na kukusanya kodi, ushuru na ada mbalimbali kwa jinsi sheria za Nchi zinavyoruhusu. Kwa hakika, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 katika kifungu cha 14, inaitaka kila Halmashauri ya Wilaya na kila Mamlaka ya Mji (Halmashauri ya Mji, Manispaa au Jiji) kutoza na kukusanya kodi na mapato mengine ambayo yatatosheleza matumizi yaliyoidhinishwa. Hilo ni jukumu la kimsingi ambalo sheria imezipa Serikali za Mitaa, lengo likiwa ni kuhakikisha zinapata fedha za kutosha ili ziweze kutoa huduma kwa viwango vilivyowekwa.

3. Kutokana na hayo, moja ya malengo mahsusi ya Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa, ni kuongeza mapato na rasilimali za mamlaka za Serikali za Mitaa na kuinua ufanisi katika matumizi ya mapato na rasilimali hizo. Chini ya Programu hiyo imepangwa kuwa Halmashauri zitaongeza jitihada za kukusanya mapato kutokana na vyanzo vyao vya mapato na pia kwamba ruzuku kutoka Serikali Kuu itaongezeka kwa kiasi kikubwa ili ipate kulingana na kazi za Halmashauri. Lakini upande mwingine ni kwamba usimamizi wa matumizi ya mapato na rasilimali hizo utaimarishwa ili Wananchi waweze kupata thamani ya fedha wanazolipa kama kodi, ushuru na ada mbalimbali kutokana na wingi na ubora wa huduma watakazopata.

**Vyanzo vya Mapato ya Halmashauri**

4. Halmashauri hupata mapato yake kutoka vyanzo kadhaa ambavyo vinagawanyika katika makundi mawili makubwa kama ifuatavyo:

   (i) Vyanzo vya Halmashauri yenyewe
   (ii) Ruzuku kutoka Serikali Kuu

5. Halmashauri za Miji na Wilaya hukusanya mapato kutokana na vyanzo vyao ambavyo kwa sehemu kubwa yanaangukia katika makundi matatu kama ifuatavyo:

   (a) Kodi mbalimbali, kwa mfano, kodi ya majengo kodi ya huduma; na kodi ya ukodishaji wa rasilimali za Halmashauri

   (b) Ushuru mbalimbali unaotozwa na Halmashauri kwa mfano, ushuru wa mazao, ushuru wa mifugo n.k.

   (c) Ada mbalimbali zinazotozwa na Halmashauri kama njia za kuruhusu uendeshaji wa shughuli yoyote ya kiuchumi au kijamii katika eneo la Halmashauri kwa mfano, ada za leseni za biashara, ada za uandikishaji wa teksi na magari ya kubeba abiria mijini, ada za leseni za vileo, n.k. Aidha, ada hutozwa kutokana na huduma zinazotolewa kwa mfano, ada ya kuogesha mifugo, ada ya kutumia gari la wagonjwa (ambulance) n.k.

6. Pamoja na kujitahidi kuboresha ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo mbalimbali vya Halmashauri yenyewe ilibidi kuchunguza uwezekano wa kupunguza idadi ya vyanzo vya mapato ya Halmashauri. Hii ni kwa vile baadhi ya kodi zilizokuwa zinatozwa kwa gharama kubwa, zilikuwa haziingizi mapato ya kuridhisha na nyingine zilikuwa zinasababisha bughudha tu kwa Wananchi. Kwa hiyo chini ya Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa, kila Halmashauri ilipata fursa ya kuchambua vyanzo vyake vya mapato kwa lengo la kufuta vile ambavyo gharama ya kukusanya mapato ni kubwa kuliko mapato yaliyokuwa yakipatikana; au vile ambavyo utozaji wake ulikuwa chanzo cha kero na bughudha kwa Wananchi, ili kuepusha Halmashauri kufarakana na walipa kodi wake.

7. Kwa upande wa ruzuku kutoka Serikali Kuu, tangu mwaka 1984 hadi 1999/2000 Serikali imekuwa ikitenga ruzuku kwa Halmashauri za Miji na Wilaya katika bajeti yake ya kila mwaka kwa ajili ya huduma za elimu. Kuanzia mwaka wa fedha 2000/01 Serikali ilianza pia kutenga ruzuku kwa ajili ya huduma za kilimo na mifugo. Huduma hizi ni nyeti na zikiboreshwa zinaweza kusaidia sana katika mapambano dhidi ya umaskini. Ndiyo maana Serikali imekuwa ikitoa ruzuku na pia Halmashauri zimekuwa zikihimizwa zichangie fedha kutoka vyanzo vyao vya mapato ili kuziba pengo pale ambapo ruzuku kutoka Serikalini haitoshelezi mahitaji.

8. Utaratibu umeandaliwa chini ya Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa wa kuzipatia Halmashauri ruzuku za jumla za kisekta (Sectoral block grants) kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika sekta husika kwa kutumia vigezo maalum. Lengo ni kuiwezesha Halmashauri yenyewe kupanga na kuamua itakavyotumia ruzuku hiyo kulingana na vipaumbele na mahitaji yake, na kwa kuzingatia sheria na sera za taifa pamoja na mazingira ya Halmashauri yenyewe badala ya kupangiwa na Serikali. Inatarajiwa kuwa kwa utaratibu huu, mpango na bajeti ya Halmashauri vitakuwa na wenyewe, hali ambayo itawafanya Wananchi wapende kushiriki katika kupanga na kutekeleza mipango yao ikiwa ni pamoja na kulipa kodi na ushuru mbalimbali ili hiyo mipango yao iweze kutekekezwa.

**Mfumo wa Kuzipatia Serikali za Mitaa Ruzuku ya Maendeleo**

9. Serikali imeandaa Mfumo wa Kuzipatia Serikali za Mitaa Ruzuku ya Maendeleo. Ruzuku itakayotolewa chini ya mfumo huu itatumiwa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na ndio utaratibu ambao hatimaye utatumiwa katika kuzipatia Serikali za Mitaa fedha za maendeleo.

10. Kwa ujumla, lengo la mfumo huu wa kuzipatia Serikali za Mitaa ruzuku ya maendeleo ni kuboresha upatikanaji wa huduma kwa jamii, hususan wale walio maskini kwa kujenga na kukarabati miundombinu, na kuinua uwezo wa usimamizi na utendaji kazi kwa ujumla. Serikali imeamua kuweka uhusiano kati ya upatikanaji wa fedha na kiwango cha utendaji katika Halmashauri kuhusu usimamizi wa fedha, uandaaji wa mipango

shirikishi, uandaaji wa bajeti zinazozingatia hali ya umaskini ilivyo katika halmashauri na masuala mapana ya utawala bora yanavyohusu uwazi na uwajibikaji na ushirikishwaji wa ngazi za chini za Serikali za Mitaa.

11. Katika hali hiyo, fedha za maendeleo zitatolewa tu kwa Halmashauri zitakazothibitika kuwa zimetimiza masharti ambayo kwa ujumla yanahusu utawala bora, kwa mfano Halmashauri isiwe imepata hati chafu ya ukaguzi kwa hesabu zake za mwaka uliotangulia.

12. Kwa kuanzia, mfumo huu mpya utapatiwa fedha na Benki ya Dunia kwa ajili ya Halmashauri 41 wakati Halmashauri zilizosalia zitapatiwa fedha za maendeleo kutoka Serikali ya Tanzania na Mfuko wa Pamoja ulioundwa na Wahisani, lakini fedha zote hizi zitatoka kwenye mfuko mkuu wa Serikali unaosimamiwa na Wizara ya Fedha.

**Matumizi ya Fedha za Serikali za Mitaa**

13. Matumizi ya fedha za Halmashauri ambazo zinatokana na vyanzo vyao vya mapato na ruzuku kutoka Serikali Kuu, yanatakiwa yapangwe kwa namna ambayo itawezesha utoaji wa huduma muhimu kwa wingi na ubora unaotakiwa. Matumizi hayo yanatakiwa yalenge katika kuiwezesha Halmashauri kutekeleza sheria na sera za Serikali kama zinavyoainishwa katika mwongozo wa kitaifa wa maandalizi ya mpango na bajeti ambao hutolewa kila mwaka, pamoja na mwongozo maalum unaotolewa kwa Serikali za Mitaa na Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa kufuatia huo wa kitaifa.

14. Ili kuhakikisha kuwa mpango na bajeti ya Halmashauri vinazingatia vipaumbele na mahitaji halisi ya Wananchi, ni muhimu mipango iandaliwe kuanzia chini kwenda juu na Wananchi washirikishwe huko huko walipo (ngazi ya kitongoji, kijiji na mtaa) kwa kutumia mbinu shirikishi za kuandalia mipango. Itabidi pia wajulishwe kuhusu mpango wa Halmashauri kama ilivyoidhinishwa ili waweze kushiriki katika kuutekeleza.

15. Taratibu za fedha kuhusu ruzuku za jumla (block grants) za mwaka 2000, zinazitaka Halmashauri kutenga fedha katika bajeti ya mwaka kwa kila kituo cha huduma kilichoko katika eneo la Halmashauri (shule

ya msingi, zahanati, kituo cha afya, skimu ya maji, kituo cha huduma za wakulima n.k.) na pia kuhakikisha kuwa kumbukumbu zinawekwa juu ya vifaa vinavyonunuliwa na kupelekwa kwenye vituo hivyo. Utaratibu huu utaiwezesha Halmashauri kujua ni kwa kiasi gani, na kwa ubora gani, huduma zinawafikia walengwa. Pia utawezesha upatikanaji wa huduma wenye kuzingatia haki na usawa.

**Uidhinishaji wa Mpango na Bajeti**

16. Kabla Halmashauri (Full Council) haijawasilishiwa mpango na bajeti, rasimu yake itapelekwa mkoani ambako Sekretarieti ya Mkoa itachambua na kuhakikisha kuwa mpango na bajeti kweli vimezingatia sera za kisekta, sheria na maelekezo yaliyomo katika mwongozo wa kitaifa wa kuandaa mipango na bajeti. Sekretarieti hiyo itamwandikia Mkurugenzi wa Halmashauri maoni kuhusu rasimu ya mpango na bajeti. Mkurugenzi pamoja na timu yake ya menejimenti itafanya marekebisho kwa jinsi itakavyoonekana inafaa na inastahili, na kuwasilisha kwenye Kamati ya Halmashauri inayohusika na masuala ya fedha na kisha kwenye kikao cha Halmashauri (Full Council) kitakachoitishwa maalum kwa ajili ya kujadili na kuidhinisha Mpango na Bajeti ya mwaka.

17. Bajeti iliyoidhinishwa ni sehemu ya sheria. Yeyote anayekwenda kinyume cha bajeti iliyoidhinishwa anavunja sheria na anapaswa kushughulikiwa kama sheria na taratibu zinavyoelekeza. Ni muhimu kutaja hapa tahadhari iliyopo katika kifungu cha 116(4) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Na.7 ya mwaka 1982 na kifungu cha 58(4) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Na.8 ya mwaka 1982 kama zilivyorekebishwa na Sheria Na.6 ya mwaka 1999 kwamba ikiwa Madiwani watatumia vibaya madaraka yao katika kikao au vikao vyao, kwa mfano kuamua fedha za Halmashauri zitumiwe kwa madhumuni yasiyokusudiwa, wanaweza kushtakiwa chini ya kifungu cha 96 cha Sheria ya Adhabu Sura ya 16.

**Udhibiti wa Fedha za Halmashauri**

18. Kwa muhtasari, wajibu wa Madiwani katika udhibiti wa fedha za Halmashauri ni kama ifuatavyo:

(a) Kuhakikisha kuwa matumizi ya Halmashauri hayavuki viwango vilivyoidhinishwa

(b) Kuhakikisha kuwa fedha za Halmashauri zinasimamiwa kwa mujibu wa kanuni na taratibu zilizowekwa na kwa kuzingatia maelekezo ya Serikali

(c) Kuhakikisha kuwa sheria ndogo zinazohusu ukusanyaji wa mapato zinaandaliwa na kuidhinishwa mapema na kwamba mapato yote yaliyokadiriwa yanakusanywa kulingana na bajeti iliyoidhinishwa

(d) Kuhakikisha kuwa Wananchi wanapata thamani ya fedha kwa njia ya huduma bora kutokana na fedha wanazolipa kama kodi, ushuru na ada mbalimbali

(e) Kusimamia utekelezaji wa miradi inayotekelezwa chini ya mpango wa maendeleo wa Halmashauri

(f) Kuhakikisha kuwa taarifa za fedha za Halmashauri zinawafikia Wananchi na kuzielezea katika Kamati za Maendeleo za Kata ili zieleweke vilivyo

(g) Kuchambua taarifa za fedha za robo mwaka na mwisho wa mwaka na kuelekeza hatua za kuchukuliwa ili kuimarisha hali ya kifedha ya Halmashauri

(h) Kuzingatia taarifa za ukaguzi wa ndani na nje na kuhakikisha kuwa ushauri na maelekezo yaliyomo yanashughulikiwa vilivyo

(i) Kuhakikisha kuwa hesabu za Halmashauri zinafungwa kwa wakati uliowekwa na sheria

(j) Kupitia na kujiridhisha juu ya majibu ya hoja za ukaguzi na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kuhusu hesabu za Halmashauri

(k) Kuhakikisha kuwa matumizi ya fedha yanafuata bajeti ya Halmashauri

(l) Kutunza mali na vifaa vya Halmashauri ili viweze kutoa huduma endelevu.

19. Ili kuhakikisha kuwa udhibiti wa fedha za Halmashauri unatekelezwa inavyopasa, kutakuwepo Kamati ya Halmashauri itakayoshughulikia masuala ya fedha ambayo itakuwa inakutana kila mwezi na wajibu wake utakuwa ni kufuatilia utekelezaji wa majukumu yote yaliyotajwa hapo juu. Hata hivyo, ni muhimu kusisitiza kuwa usimamizi wa siku hadi siku wa fedha za Halmashauri utakuwa

jukumu la Mkurugenzi na wasaidizi wake ambao wanapaswa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizoidhinishwa na kutolewa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kwa ajili ya usimamizi wa fedha.

**Mwisho**

20. Umuhimu wa Halmashauri kuwa na fedha pamoja na rasilimali nyingine unastahili kusisitizwa. Ni muhimu pia kuhakikisha kuwa matumizi ya fedha hizo yanadhibitiwa ili fedha zisitumiwe kwa madhumuni yasiyokusudiwa. Kwa kifupi, Halmashauri yenye fedha za kutosha na ambayo inasimamia vizuri na kudhibiti matumizi ya fedha zake ndiyo itakayoheshimiwa na walipa kodi na pia kustahili ushirikiano na msaada wa washika-dau wengine katika ngazi mbalimbali. Ndiyo maana Kamati ya Halmashauri inayoshughulikia masuala ya fedha inatakiwa kukutana kila mwezi ili kuzingatia mwenendo wa hali ya fedha ilivyo katika Halmashauri na kuchukua hatua zifaazo mapema.

21. Kwa hiyo, ni muhimu Halmashauri ihakikishe inakusanya mapato yote yanayostahili na kuyatumia mapato hayo katika kuboresha utoaji wa huduma. Ni kwa njia hii tu, Wananchi wanaweza kuvutiwa kulipa kodi na ushuru wa Halmashauri. Watakata tamaa ikiwa watahisi kuwa fedha wanazolipa kama kodi zinaishia mifukoni mwa watu wachache wakati utoaji wa huduma unazidi kuzorota.

______________x________________x___________________